

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII**

Anwani ya Simu "AFYA", DAR ES SALAAM  
SimuNa.:255 – 022 - 2120261 – 7  
Fax Na. 255 -022- 2139951  
(Barua zote ziandikwekwa KatibuMkuu)



S.L.P. 9083  
**DAR ES SALAAM**

**Unapojibutafadhalii taja:**

Kumb. Na. **GA.16/209/01C/70.**

**20 Septemba, 2013**

**Makatibu Tawala Mkao,  
Tanzania Bara.**

**Waganga Wakuu wa Mikoa,  
Tanzania Bara.**

**Wakurugenzi wa Hospitali za Rufaa,  
Tanzania Bara.**

**Waganga Wakuu wa Wilaya,  
Tanzania Bara.**

**YAH: MABADILIKO KATIKA MATUMIZI YA DAWA ZA  
KUPUNGUZA MAKALI YA UKIMWI NCHINI**

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI inasimamia na kuratibu utoaji wa huduma za Matunzo na Tiba ikiwemo kuhakikisha upatikanaji wa dawa bora za kupunguza makali ya UKIMWI (ARVs) na vifaa husika kwa matumizi ya Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU).

Kutokana na tafiti mbalimbali, ushauri wa kisayansi sambamba na mapendekezo ya Shirika la Afya Duniani (WHO), Wizara imeamua kutoa Waraka huu ikiwa ni jitihada za kuboresha matibabu kwa WAVIU.

Waraka huu umezingatia kurekebisha orodha ya dawa za kupunguza VVU kwa watu wazima kama ifuatavyo:-

1. WAVIU wote wapya wanaoanzishiwa dawa, watumie dawa aina ya Tenofovir 300mg/Lamivudine 300mg/Efavirenz 600mg (TDF300mg / 3TC300mg EFV600mg) na itakuwa dawa ya chaguo la kwanza katika kundi la dawa za mstari wa kwanza.
2. WAVIU wote watu wazima wasioweza kustahimili dawa ya chaguo la kwanza, watumie dawa mbadala katika kundi la mstari wa kwanza ambazo ni Zidovudine 300mg/ Lamivudine 150mg + Efavirenz 600mg, Zidovudine 300mg Lamivudine 150mg/ Nevirapine 200mg na Tenofovir 300mg/ Emtricitabine 200mg/ Efavirenz 600mg. Pia dawa hizi zitatumika kwa WAVIU wapya ambao watashindwa kustahimili dawa ya chaguo la kwanza.
3. Dozi mchanganyiko zenyetumike dawa aina ya Abacavir zitumike tu kwa WAVIU watakaoshindwa kustahimili dawa mchanganyiko ya Tenofovir na Zidovudine na itumike katika dozi mchanganyiko za kundi la mstari wa pili.

Wizara inasisitiza kuwa dawa hizi zinapatikana Bohari ya Dawa (MSD) kwa hiyo, vituo vyote vya afya vinavyotoa huduma za matunzo na tiba kwa WAVIU vizingatie mabadiliko haya ili kuboresha huduma.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na *Dkt. Robert Mwanri Josiah* simu namba +255 22 2131 213, barua pepe:[rmwjosiah@gmail.com](mailto:rmwjosiah@gmail.com)

Nashukuru kwa ushirikiano wako.

*luisinde*  
Dkt. Doñan W. Mmbando  
**KAIMU KATIBU MKUU**